

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



19 SEPTEMBER, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA TANO – TAREHE 19 SEPTEMBER, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Maelezo ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 [*Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004*].

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya

Mwaka 2004 [*Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004*].

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

68. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, nini mpango wa kuhakikisha Madereva wa magari ya abiria na mizigo wanapewa mikataba ya kazi ili kupata mafao na Bima za Afya.



WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

69. MHESHIMIWA BENAYA LIUKA KAPINGA (MBINGA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatenga fedha za ujenzi wa Vituo vya Afya Kata za Ukata na Litumbandyosi Halmashauri ya Wilaya Mbinga.

**70. MHESHIMIWA YUSTINA ARCADIUS RAHHI
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna manufaa gani ya kuunganisha Idara ya Kilimo na Mifugo katika Halmashauri za Wilaya.

**71. MHESHIMIWA MOHAMED LUJYO MONNI
(CHEMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itawalipa Watumishi waliohamishiwa katika Halmashauri ya Chemba.

WIZARA YA MAJI:

**72. MHESHIMIWA MWANTUM MZAMILU ZODO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha Mradi wa Maji wa Vuga – Mlembule katika Mji Mdogo wa Mombo Wilayani Korogwe.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

**73. MHESHIMIWA MOHAMED SAID ISSA
(KONDE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji,
Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wigo
wa biashara baina ya Zanzibar na Tanzania
Bara ili kuongeza mapato.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**74. MHESHIMIWA AMOUR KHAMIS MBAROUK
(TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, kuna Wavumbuzi wangapi na wa teknolojia
gani kwani Mpango wa 3 wa Maendeleo ya
Taifa una lengo la kuchochea uvumbuzi.

**75. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI
(TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu,
Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini Darasa la 7 wanafanya Mtihani wa
Taifa Mwezi wa 9 huku Mtaala unaelekeza
masomo yakamilike mwisho wa Mwaka.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**76. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA
(KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na
Utalii:-

Je, ni lini Serikali itawaondoa Wananchi
waliovamia Msitu wa Bondo uliopo Kata ya
Mswaki, Kijiji cha Mswaki.

WIZARA YA KILIMO:

**77. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA
SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni kwa nini Wakulima wasianze kujua bei ya kuuzia Tumbaku na bei ya pembejeo kabla ya kufunga Mkataba wa uzalishaji.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

78. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

- Je, ni yapi yalikuwa malengo ya Serikali kuanzisha Chuo cha Diplomasia.

WIZARA YA AFYA:

79. MHESHIMIWA BUPE NELSON MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Rukwa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**80. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, kuna mpango gani wa kurekebisha Ramani
ya nchi yetu baada ya baadhi ya maeneo
kujazwa mchanga kuongeza ukubwa wa ardhi.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**81. MHESHIMIWA KENNETH ERNEST NOLLO
(BAHI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na
Sheria:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuleta Mikataba ya
Madini na Nishati ijadiliwe Bungeni kabla ya
kuingia makubaliano na Wawekezaji.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

82. MHESHIMIWA ZAHOR MOHAMMED HAJI (MWERA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali inaweza kutoa idadi na aina ya mikopo ya Zanzibar baada ya makubaliano na kuiwezesha Zanzibar kukopa yenyewe.

83. MHESHIMIWA ORAN MANASE NJEZA (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Mfuko uliopo BOT wa Trilioni moja kutoa dhamana kwa Waagizaji mbolea kwa njia ya *Hedging/options*.

84. MHESHIMIWA OLIVER DANIEL SEMUGURUKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itafungua Matawi ya Benki ya Kilimo katika Wilaya za Mkoa wa Kagera.


IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha wa Mwaka 2022 [*The Written Laws (Financial Provisions) (Amendments) Bill, 2022*].

V. HOJA ZA SERIKALI:

MAAZIMIO:



WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Mkataba wa Umoja wa Nchi Huru za Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Ugaidi ya Mwaka 2004 [*Protocol to the OAU Convention on the Prevention and Combating of Terrorism, 2004*].

**DODOMA
19 SEPTEMBER, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**